

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA TATU**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA AROBAINI NA TANO**

**17 JUNI, 2016**

## **MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA AROBAINI NA TANO**

**TAREHE 17 JUNI, 2016**

### **I. DUA:**

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt.Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

#### **Makatibu Mezani:**

1. Ndg. Lawrence Makigi
2. Ndg. Asia Minja

Baada ya kusoma Dua Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walitoka nje.

### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

- Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu malalamiko yaliyofikishwa kwenye Kamati dhidi ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutuhumiwa kusema uongo na kutoa taarifa ambazo hazina ukweli Bungeni.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Swali Na.379 – Mhe. Raphael Masunga Chegeni [kny. Mhe. Freeman Mbowe]

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Raphael Masunga Chegeni  
(ii) Mhe. Venance Methusala Mwamoto  
(iii) Mhe. Mary Pius Chatanda  
(iv) Mhe. George Huruma Mkuchika

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na.380 – Mhe. Almas Athumani Maige

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Almas Athumani Maige  
(ii) Mhe. Augustino Manyanda Masele  
(iii) Mhe. Martha Moses Mlata

Swali Na.381 Mhe. Rashid Mohammed Chuachua

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Rashid Mohammed Chuachua  
(ii) Mhe. Moshi Suleiman Kakoso  
(iii) Mhe. Richard Philip Mbogo

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Swali Na.382 – Mhe. Margareth Simwanza Sitta

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Margaret Simwanza Sitta  
(ii) Mhe. Daniel Edward Mtuka  
(iii) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate

Swali Na.383 – Mhe. Oliver Daniel Semuguruka [kny. Mhe. Savelina Mwijage]

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Oliver Daniel Semuguruka  
(ii) Mhe. Omary Tebweta Mgumba

Swali Na.384 – Mhe. Dkt. Faustine Englebert Ndugulile

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Dkt. Faustine Englebert Ndugulile  
(ii) Mhe. Ally Keissy Mohamed  
(iii) Mhe. Fakharia Shomar Khamis  
(iv) Mhe. Joseph George Kakunda

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Swali Na.385 – Mhe. Halima Abdallah Bulembo [kny. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru]

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Halima Abdallah Bulembo  
(ii) Mhe. Boniface Mwita Getere

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Swali Na.386 – Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni  
(ii) Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa  
(iii) Mhe. Emmanuel Papian John  
(iv) Mhe. Cosato David Chumi

Swali Na.387 – Mhe. Josephat Sinkamba Kandege

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Josephat Sinkamba Kandege  
(ii) Mhe. Constantine John kanyasu  
(iii) Mhe. Ignas Aloyce Malocha  
(iv) Mhe. Dkt Dalaly Peter Kafumu

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na.388 – Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Azza Hilal Hamad  
(ii) Mhe. Martha Jachi Umbulla

#### **IV. MATANGAZO:**

1. Wageni wote waliokuwepo Bungeni walitambulishwa.
2. Kamati ya Katiba na Sheria ilitangaziwa kukutana kwa Kikao.
3. Semina kuhusu Mazingira itakayotolewa na LEAD FOUNDATION – itafanyika Jumamosi tarehe 18/6/2016 kuanzia saa 4.00 asubuhi Ukumbi wa Pius Msekwa.
4. Siku ya Jumapili tarehe 19/6/2016 kutakuwa na Semina kuhusu procurement Bill.

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

Mhe. Livingstone Joseph Lusinde alitumia kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo kuhusu Wabunge Waislam wa UKAWA kugomea futari kwa msingi/madai kwamba imeandaliwa na Naibu Spika jambo ambalo siyo kweli kwani iliandaliwa na Waziri Mkuu na kutaka kujua lipi bora kati ya dini na mazoezi kwani Wabunge hao Waislam huonekana kufanya mazoezi na Naibu Spika. Kiti kilitolea maelezo kwamba kwa vile jambo hilo halijatokea Bungeni hivyo hakuna mwongozo wakutolea majibu kwa vile suala la futari halijatokea Bungeni.

#### **V. HOJA ZA KAMATI:**

Mhe. Almas Athumani Maige aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Mhe. Susan Anselm Lyimo na Mhe. Anatropia Theonest Lwehikila kutuhumiwa kusema uongo na kutoa taarifa ambazo hazina ukweli ambapo Mhe. Susan Anselm Lyimo Kamati ilipendekeza asihudhurie na Mhe. Anatropia Theonest Kamati ilipendekeza asimamishwe Vikao vitatu (3) vya Bunge. Hoja iliungwa mkono kwa mujibu Kanuni ya 63(8) kiti kilikubaliana na adhabu za Kamati.

#### **VI. KUAHIRISHA BUNGE**

Saa 5.30 Naibu Spika aliahirisha Bunge hadi Jumatatu tarehe 20/6/2016 saa 3.00 Asubuhi.

**DODOMA**  
**17 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**  
**KATIBU WA BUNGE**